

USIKATE MIGUU KWA KUTEGEMEA GARI

18 Julai, 2020



Usikate miguu kwa kutegemea gari sababu miguu ina uwezo wa kukusaidia kufanya shughuli mbalimbali na matokeo yake ukapata au kununua gari. Lakini gari haiwezi kufanya shughuli yeyote itakayokuwezesha ukapata au kuota miguu. Imezidi utaweza kununua miguu ya bandia. Hivyo hata kama unauwezo wa kununua gari ya gharama kubwa dunia, ni vema ukaendelea kuheshimu miguu yako au kuwaheshimu wanaotembea kwa miguu sababu thamani ya miguu ni ya juu kuliko gari yako.

TAAMULI

Kuna watu utakuta wanapita barabarani na kuwamwagia watu maji machafu yaliyotuama kwenye madimbwi, hadi unajiuliza; kama gari yake ya thamani kuliko watu au yeye mwenyewe ni wathamani kubwa? Kama ndivyo, huku kwenye madimbwi na makorongo kafuata nini?

Wapo Watanzania wenye tabia ya kudharau kwao na kuthamini maeneo ya wenzao yaliyoboreshwa. Nyumbani kwao wanakuona ni, "kwa kishenzi!" Hivyo kuacha kukutengeneza au kukuwekea mipango madhubuti ya kuendeleza maeneo hayo.

Lakini huko waendako, wanakokupenda ambako watu wengine kama wao walikuendeleza kukigeuka chini juu na juu chini, utawaona wanarudi nyumbani kichwa chini na kujinyenyekeza.

Watu hawa ni wanafiki na roho mbaya, wanajidhirisha pale watakapofika nyumbani nakujifanya wanataka kutoa msaada wakati nyuma ya pazia wao ndiyo wanaoomba msaada. Wapo wengi sana mwaka huu, kutokana na matokeo ya Daktari John P. Magufuli kukaza vyuma.

Wapo wengine wanaojifanya kukata miguu kwa kutegemea magari. Wanaponda sana asili yao, nyenzo zao, malezi yao, ujasiri wao na utajiri wao kwa kutegemea kile walichonacho sasa.

Kama ulilelewa kwenye uovu na wewe ukaelimika na kuwa mwema, unaponda vipi asili yako badala ya kurekebisha mifumo kama inawezekana? Kama haiwezekani, acha hivyo hivyo!

Kama wewe ulizaliwa na kulelewa na watu wadhulumat na baadae ukajitambua na kuacha kuchukua tabia hizo mbaya tambua muda ukifika na wenzako watajitambua vilevile. Nadhani muda huo umeshafika.

Tuchague viongozi wenye uwezo wakuimarisha uchumi wa kati. Tanzania ya Viwanda, inawezekana.